

Learning by Ear 2011 – Mikinzano na utatuzi – “Palipo na wazee”
Kipindi cha 2: “Mizozo na utatuzi-palipo na wazee”
Episode 2: “Tujihami”
AUTHOR: Chrispin Mwakideu
EDITOR: Andrea Schmidt, Aboubakary Liongo

List of characters by scenes:

Narrator (m/f 30-40)

SCENE ONE : MITUMBA AND HIS DAUGHTERS BY THE RIVER

- **Mitumba (m, 50)**
- **Lela (f, 20)**
- **Lela (f, 20)**

SCENE TWO : OUT IN THE OPEN FIELDS

- **Lawi (m, 20)**
- **Gulu (m, 17)**
- **Dere (m, 40)**

SCENE THREE: MITUMBA VISITS MASAMBO

- **Mitumba (m, 50)**
- **Nina (f, 40)**

SCENE FOUR: GULU AND LAWI RETURNING HOME FROM GRAZING

- **Masambo (m, 50)**
- **Nina (f, 40)**
- **Lawi (m, 20)**
- **Gulu (m, 17)**

Msimulizi

INTRO:

Hujambo na karibu katika kipindi chetu cha Noa bongo! Jenga maisha yako. Tuko katika kipindi chetu cha pili kinachoangazia mizozo na utatuzi, isimu yake, “**Palipo na wazee**”. Katika kipindi chetu cha kwanza, kwa kifupi tulikutana na familia ya Mitumba na ya Masambo. Familia hizi ziliishi bonde la Kijani, lakini walitoka kwenye misingi tofauti ya kikabila. Pia tuliona, mfano mmoja wa jinsi wa Torube wanavyoweza kupata mapatano baada ya vita. Tukaishilia na Mitumba na mabinti zake wakiwa na hamaki kwa yale walioyaoana yamefanywa shambani mwao. Haswa ni nini? Sikiliza kwa makini tung’amuliwe katika kipindi cha leo, kinachoitwa, “**Tujihami**”. Na tunaanzia pale kwa Mitumba na binti zake karibu na mto.

SCENE ONE: MITUMBA AND HIS DAUGHTERS BY THE RIVER

1. SFX: WATER FLOWING IN A RIVER

- 2. LELA:** Tutafanyaje baba?
- 3. SHANI:** Wakiendelea kuziba maji yasifike shambani kwetu basi mimea itakauka na hatutakuwa na kitu cha kuvuna baada ya kazi ngumu ya ukulima tunayofanya.
- 4. LELA:** Hatuwezi kutegemea mvua pekee. Ni lazima tupate maji ya mto pia.
- 5. MITUMBA:** (**Furious**) Munafikiria sijui matokeo ya huu uhasama? Lela, nenda kaliondoe lile jiwe linaloziba mto usilete maji shambani. Tusifanye hasira.

- 6. SHANI:** Lakini kutoa jiwe haisaidii kitu baba!
- 7. LELA:** Ndio, wa Masambo wanafikiria watatufanya sisi maziwa lala.
- 8. MITUMBA:** Sssh! Lela, fanya kama nilivyokuamuru.
Nitazungumza na wa Masambo. Lela! Fanya hivyo.
(Lela acts out lifting heavy rock)
- 9. MITUMBA:** Shani, nenda ukamsaidie dadako..
(Lela and Shani act out lifting heavy rock together)
- 10. LELA:** **(Takes a deep breath)** Aii..hili jiwe ni zito kushinda walilozibia wakati ule.
- 11. SFX: STREAM OF WATER FLOWING**
- 12. MITUMBA:** Sawa. Maadamu maji yamerudi kuingia shambani, nasi turudini kuendelea kulima.
- 13. MSIMULIZI:** Mitumba alifanya busara kutowacha hasira ziwatawale.
Tukirudi kule malishoni, Lawi na Gulu walivuka mpaka wa ngambo ya pili kutafuta nyasi za kulishia ng’ombe, zahama ikazuka. Walijikuta wamezingirwa na wezi wa ng’ombe wa Kimbebe, kundi haramu la kikabila lililo jihami kwa silaha likiongozwa na Dere. Tega sikio zaidi.

14. SCENE TWO: OUT IN THE OPEN FIELDS

15. SFX: COWS AND GOATS MAKING SOUNDS

16. SFX: TWO PEOPLE WALKING THROUGH THE FIELDS

17. GULU: **(afraid)** Lawi, unafikiria bado tuko maeneo yetu?

- 18. LAWI:** Usiogope Gulu, wa Torube si watu waoga. Hutaki kuja kuwaeleza watoto na wajukuu wako kuhusu masaibu yako?
- 19. GULU:** Nataka, lakini ni hapo kama nitakua hai kuwahadithia.
- 20. LAWI:** Gulu, wewe una maono mabaya. Afadhali kama ungeliwaza kupata kwetu nyasi nzuri za kulishia mifugo yetu. Alafu labda tungelihama bonde hili la Kijani.
- 21. GULU:** Alafu tuwaachie kila kitu wa Koroma? Haiwezekani! Unajuwa nini? Baada ya ng’ombe wetu kumaliza kunywa maji, niliweka jiwe kubwa kuwazuia wa Koroma wasiibe maji yetu. Nafikiri, safari hii hawataweza kuliondoa.
- 22. LAWI:** Gulu, wacha kufanya hivyo. Hicho kitu kidogo kinaweza kuleta mkinzano mkubwa.

23. SFX: CAMELS APPROACHING AT A FAST PACE

- 24. LAWI:** **(Shouts)** Kimbia! Gulu! Kimbia! Hawa ni wezi wa mifugo kutoka Kimbebe!
- 25. GULU:** **(afraid)** Lakini..Lakini na wewe? Na ng’ombe?
- 26. LAWI:** **(desperate)** Usijali juu yangu na ng’ombe. Wewe kimbia na ujifiche! Haraka, wanatukaribia.
- 27. GULU:** **(almost in tears)** Lawi, siwezi kukuwacha peke yako. Nitabaki nikusaidie kupigana.

28. SFX: CATTLE START TO MAKE SOUNDS UNCONTRALLABLY

29. LAWI: La! hatuwezi kupigana na wezi hawa wa mifugo wa Kimbebe kwa mikuki na mishale. Wao wana silaha ambazo jeshi letu wako nazo. Sasa nenda!

30. SFX: CAMELS RIDING NOW EVEN LOUDER AND CLOSER

31. DERE: **(motions for the rest to stop)** Eish! Kila mtu asimame.

32. LAWI: **(Coughing from the dust)** Dere, mkuu wa Kimbebe, tafadhali usiniue.

33. DERE: Uko peke yako, kwenye maeneo yetu?

34. LAWI: Ndio, babangu ni mzee , na mimi ni kijana wake wa pekee. Bonde la Kijani halina tena nyasi. Ndio nikaja mbali huku kote kutafuta malisho ya ng’ombe.

35. DERE: Una hakika huu sio mtego? Sema ukweli, ukitaka nikuwachilie. Wenzako wako wapi? Kawaida munatembea makundi makundi.

36. LAWI: Niko peke yangu na hawa ng’ombe wa babangu.

37. DERE: Sawa. Nitachukua ng’ombe peke yake, na nikuwache hai. Jamaa! Tupelekeni ng’ombe Kimbebe.

38. LAWI: **(shouts)** La! swezi kuwaruhusu muchukue ng’ombe wote. Itwabidi pia mimi munichukue au muniue.

39. DERE: **(Laughs out)** Kwa hivyo ni kweli utamaduni wenu unavyosema. Wapiganiaji wa Torube hamuogopi kifo!

Umenivutia sana. Na kwa vile leo nina raha,
tutachukuwa ng’ombe idadi nusu.

40. LAWI: (breathes a sigh of relief) Asante.

41. DERE: Usinishukuru. Shukuru mababu zako waliokulinda siku
ya leo (calls out) Sawa, watu wangu! Chukueni nusu
ya ng’ombe hao! Nusu eh! Twendeni!

42. SFX: CATTLE MOOING LOUDLY

43. MSIMULIZI: Mikinzano ni kitu cha kawaida kwa wa Afrika. Watu
wamekosana na wamepigana tangu jadi , lakini kidogo mambo yaligeuka
tangu bunduki na silaha otomatiki zilipozinduliwa . Kama tulivyoona na
wezi wa mifugo wa Kimbebe. Masambo atazipokea vipi taarifa hizi? Lakini
twende huko, Mitumba pia alikuwa ataka kumuona.

SCENE THREE: MITUMBA VISITS MASAMBO

44. SFX: KNOCK ON A DOOR

45. MITUMBA: Masambo! Wenyewe muko?

46. NINA: Habari Mitumba. Masambo hayuko, naitwa Nina,
mkewe. Umeletwa na nini huku kwetu?

47. MITUMBA: Nina. Yuko wapi mumewako Masambo?

48. NINA: Masambo na wavulana wangu hawako. Kwa hivyo
mimi ndiye msimamizi wa hapa kwa sasa.

49. MITUMBA: Nitarudi warudipo. Haya ni mambo yanayowahusu

wanaume.

50. NINA: Alaa, kweli? Kwanza, ni mambo yanayowahusu wanaume, na wasipoelewana inakuwa vita vya wanaume, lakini ni nani wanaotaabika zaidi? Hmm?

51. MITUMBA: Siwezi kukujibu.

52. NINA: Wewe una binti zako wawili. Mkeo aliondoka na hajarudi tena. Kwa hivyo unafaa kuwa na jibu kuliko mtu mwengine yeyote. Ni wanawake na watoto wanaotaabika.

53. MITUMBA: Sikuja hapa unikumbushe kuhusu mke wangu au familia yangu. Mueleze mumeo na wavulana wako. Nimekuwa kimya nikiwatazama kile wanachofanya. Na hii ni mara ya mwisho tunaliondoa lile jiwe. Kwaheri.

54. NINA: Jiwe gani? Eh? Mitumba, hatutaki turudie tena ile mikinzano ya watu wako na wangu. **(starts to cry)** Tuliteseka vyakutosha.

55. MITUMBA: Hukuteseka peke yako. Wahabarishe niliyokwambia. Na uwakumbushe, ukimya sio ishara ya unyonge.

56. MSIMULIZI: Dakika chache baada ya Mitumba kuondoka, Masambo aliwasili nyumbani kwake. Alitoka kwenye mkutano wa wakuu wa kabila lao. Lakini kwanza tuungane na Gulu na Lawi walipokuwa wana simanzi ya kurudi nyumbani na idadi nusu ya ng’ombe za baba yao.

SCENE FOUR: GULU AND LAWI RETURNING HOME FROM GRAZING

57. SFX: DISTANT AND FEW CATTLE MAKING SOUNDS

- 58. GULU:** Lawi, tutamweleza vipi baba. Atawaka moto akiona masalio ya ng’ombe zake.
- 59. LAWI:** Maji yashamwagika, anafaa kushukuru kuwa tumerudi salama na hawa ng’ombe wengine.
- 60. GULU:** Natumai atashukuru. Sasa ilikuwaje? Ulizungumza nao?
- 61. LAWI:** La, pale hapakuwa ni pahala pa majadiliano na muda pia haukuruhusu, Gulu. Niliawaeleza wazi, wakichukua ng’ombe zote za baba na mimi pia waniue!
- 62. GULU:** **(shocked)** Uliwaambia hivyo!
- 63. LAWI:** Wale pale nje baba na mama; hmm, itakua ngumu, hawaonekani wenye furaha.

64. SFX: EVENING AMBIENCE IN VILLAGE

- 65. MASAMBO:** **(demanding)** Ng’ombe wengine wako wapi?
- 66. NINA:** Mumewangu, watoto wetu wamekuwa malishoni siku nzima, hata hutaki kujuwa wameshinda vipi?
- 67. LAWI:** Habari baba na mama
- 68. GULU:** Habari baba.. ha..
- 69. MASAMBO:** **(Infuriated)** Nimekuuliza swali. Ng’ombe ziwapi?
- 70. LAWI:** Baba, samahani lakini nina habari mbaya.

- 71. MASAMBO:** Hapana! Nishaelezwa habari mbaya za kutosha!
Usiniambie ng’ombe zimeibiwa. Tafadhali....
- 72. GULU:** **(frightened)** Ng’o...Ng’ombe zako zimeibiwa, baba.
- 73. MASAMBO:** **(furiously mad)** Nimekwambia usiniambie ng’ombe zangu zimeibiwa.
- 74. NINA:** **(shocked)** Woiiii, Lini ? Wapi ? Nani?
- 75. LAWI:** **(Remorseful)** Ni wezi wa ng’ombe wa Kimbebe.
Walituvamia ghafla kwa ngamia wakiwa na bunduki na silaha zingine. Sikuwa na lakufanya. Samahani, baba.
- 76. GULU:** Tusamehe. Lawi alikuwa jasiri. Pia aliniokoa kwa kuniambia nijifiche.
- 77. NINA:** Nashukuru Mungu muko hai. Koma za mababu zenu zimewaokoa.
- 78. LAWI:** Hivyo ndivyo mkubwa wao alivyoniambia, wakati..
- 79. MASAMBO:** **(Still mad)** Tokeni! Nendeni mukaleta ng’ombe zangu! Hamuoni aibu kurudi hapa na ng’ombe nusu. Nje!
- 80. NINA:** **(Pleading)** Masambo, mumewangu. Punguza hamaki, ungelifurahia angalau watoto wako wamerudi salama. Kama ni ng’ombe hata sisi tutaiba nyengine.
- 81. LAWI:** Nakuahidi baba, hakika kama jua linavyotoka mashariki katika bonde la Kijani. Nitaziregesha ng’ombe zako. Nitawaeleza wapiganaji wengine na tutakwenda kulipiza kisasi.
- 82. NINA:** La.. la..la... tusizungumze juu ya visasi kwa sasa. Tafadhalini ingizeni ng’ombe zizini, na muje mule . Masambo, nakuomba kwa jina la mababu zetu.

Waache watoto waingie ndani.

83. MASAMBO: (calming down) Sawa. ingieni. Lakini haimaanishi yamekwisha. Nataka munielze kila kitu. Munieleze mulikuwa wapi, kulitokea nini na ni ng’ombe wangapi wameibiwa.

OUTRO:

Wizi wa ng’ombe ni mojawapo ya chanzo cha mizozo barani Afrika.

Masambo na wavulana wake watafanya nini baada ya kupoteza mifugo yake kwa waasi wa Kimbebe? Na kuna lipi kwa Mitumba na binti zake baada ya mzozo wa maji ya mto? Kwa haya na mengi utayapata katika kipindi kijacho cha, “**Palipo na wazee**”. Tukiangazia mikinzano na utatuzi.

Kukisikiliza tena kipindi hiki, au kutuma maoni na mapendekezo.

Tembelea tovuti yetu www.dw.de/kiswahili. Hadi wakati mwengine kwaheri kwa sasa.